**KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA (K.K.K.T)**

**DAYOSISI YA DODOMA**

**SHULE YA SEKONDARI EMBEKO**

**S.L.P 106, KONDOA**

E-mail: embekolutheran@gmail.com

Mob. 0786-853890/0764-581739

**Website.www.embeko.org**

---

Mzazi/mlezi wa……………………………………………

**YAH**: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI EMBEKO 2026

Ninafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha…………………kwa mwaka……….

Tunakupongeza sana na tunakukaribisha hapa ujiunge na jumuya nzima ya EMBEKO SEKONDARI.Hivyo nimategemeo yetu kuwa utakuwa ni mwanafunzi mwenye kujitambua mwenyewe na anayetambua umuhimu wa ELIMU

Aidha ni matarajio yetu kwamba utatumia muda vizuri wa miaka minne hapa shuleni kwa bidi,uaminifu,uadilifu, na hekima kubwa ili kujenga taifa letu.

"**HONGERA NA KARIBU SANA**"

Shule ya Sekondari ya Embeko ni shule ya mchanganyiko ya kutwa na boding iko Kondoa Mjini inayomilikiwa na Kanisa la kiinjili la Kilutheri Tanzania (K.K.K.T) Dayosisi ya Dodoma (DAD).

**Mahali shule ilipo**

Shule ya sekondari EMBEKO iko katika kata ya chemchem,Halmashauri ya kondoa mji wilaya ya Kondoa.Shule inafikika kiurahisi ,Unapotokea Jiji la Dodoma au mji wa Babati, shuka Stendi ya Bicha, Kondoa. Chukua usafiri kuelekea Kondoa Mjini,Yapata kilomita 1 kutoka Bicha stendi , upande wa kushoto, utaiona Shule ya Sekondari ya Embeko sambamba na Lutheran Center (Zahanati ya EMBEKO).

**Muhimu**: Mzazi/Mlezi na mwanafunzi someni kwa umakini kanuni na taratibu za shule.Mzazi/Mlezi msisitize mwanao azifanyia kazi na kisha akiri kuwa ataziishi na kuzitii kwa kipindi chote akiwa mwanafunzi wetu.

……………………………

**Siara.c**

**Mkuu wa shule**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA KILUTHERI EMBEKO
S.L.P 106 KONDOA

## KARO (ADA) NA MICHANGO MINGINE

1. **ADA**

Mwanafunzi wa kutwa anatipa Tsh 1,000,000/=

Mwanafunzi wa bweni analipa Tsh 1,400,000/=

2. **MICHANGO MINGINE**

| | |
|---|---|
| Kitambulisho | 5,000/= |
| Taaluma | 10,000/= |
| Bima ya Afya | 5,000/= |
| Ukarabati | 10,000/= |
| Huduma ya kwanza shs | 10,000/= |
| Kukodi godoro kwa mwaka | 20,000/= |
| Michezo na burudani | 5,000/= |
| Mahafali | 5,000/= |
| **Jumla shs** | **70,000/=** |

| 3. MICHANGO MINGINE KWA KIDATO CHA PILI | | 4. MICHANGO MINGINE KWA KIDATO CHA NNE | |
|---|---|---|---|
| Mtihani wa Mock | 20,000 | Mtihani wa Mock | 25,000 |
| Mtihani wa taifa | 10,000 | Mtihani wa taifa | 50,000 |
| picha | 5,000 | picha | 5,000 |
| Mtihani wa CSSC | 25,000 | Mtihani wa CSSC | 25,000 |
| Likizo mwezi wa sita | 100,000 | Likizo mwezi wa sita | 100,000 |
| | | Mahafali | 20,000 |
| **JUMLA** | **160,000** | **JUMLA** | **225,0000** |

5. **MCHANGANUO WA ULIPAJI WA ADA**

Ili iwe rahisi kwa mzazi kulipa ada tumeigawa malipo kwa awamu nne kwa mwaka kama ifuatavyo

| WANAFUNZI WA BWENI | | WANAFUNZI WA KUTWA | |
|---|---|---|---|
| Januari | 420,000 | Januari | 315,000 |
| Aprili | 350,000 | Aprili | 250,000 |
| Julai | 350,000 | Julai | 250,000 |
| Septemba | 350,000 | Septemba | 250,000 |
| **JUMLA** | **1,470,000** | **JUMLA** | **1,065,000** |

***Michango mingine ya sare,likizo mwezi Juni na mitihani ya Taifa kwa Kidato cha Pili na Nne haijajumuishwa.***

Ada na michango yote inalipwa kupitia benki ya NMB kupitia akaunti hii yenye jina la; **EMBEKO LUTHERAN SECONDARY SCHOOL,**
**AKAUNTI NAMBA 50202300954**
na kielelezo cha ushahidi wa malipo toka benki(yaani **pay-in slip**) kiletwe shuleni ili kukatiwa stakabadhi. Mzazi ajitahidi kulipa kiasi kinachotakiwa. Kwani tumeshaona madhara ya kurudisha wanafunzi nyumbani kufuatilia malipo yanavyoathiri taaluma na nidhamu ya wanafunzi pamoja na malengo ya shule kwa ujumla.

Malipo yote yafanyike kupitia akaunti hii yenye jina la;

**EMBEKO LUTHERAN SECONDARY SCHOOL, AKAUNTI NAMBA 50202300954, BENKI NI NMB**

***Kumbuka*** kuandika jina la mwanafunzi unapolipa ada na michango/kuweka fedha katika akaunti hii.

**MUHIMU**

Hakuna mwanafunzi atakayepokelewa shuleni kama hajalipa kiwango kinachotakiwa. Hata hivyo kama mzazi au mlezi atataka kulipa ada zaidi ya ilivyoainishwa anaruhusiwakufanya hivyo.

**6.** SARE ZINAZOPATIKANA SHULENI

Mzazi anapaswa kuzilipia sare zifuatazo shuleni kama atamshonea hazitakubal

| **WAVULANA** | | **WASICHANA** | |
|---|---|---|---|
| Suruali mbili za darasani | 48,000 | Sketi mbili za darasani | 48,000 |
| Suruali moja ya kushindia | 24,000 | Sketi moja ya kushindia | 24,000 |
| Sweta moja | 15,000 | Sweta moja | 15,000 |
| Tisheti mbili | 30,000 | Tisheti mbili | 30,000 |
| Traksuit moja | 30,000 | Traksuit moja | 30,000 |
| **JUMLA** | **147,000** | **JUMLA** | **147,000** |

**MAVAZI MENGINE YA LAZIMA KWA MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO**

- Viatu vyeusi vya ngozi
- Bukta moja rangi ya bluu na fulana moja rangi ya bluu zisizo na maandishi yoyote.
- Viatu vya michezo jozi moja
- Soksi ndefu za michezo rangi nyekundu josi 1
- Soksi jozi mbili au zaidi Wavulana – Nyeusi. Wasichana – Nyeupe.
- Taulo/kanga
- Shuka moja la blue na moja la pink na blanketi moja
- Shati nyeupe mbili za mikono mifupi na tai nyeusi 1
- Mkanda ya suruali kwa wavulana meusi ya bakoli ndogo isiyo na picha zozote.

**ZINGATIA**:**Mavazi mengine hayaruhusiwi.**

**7. VIFAA VYA LAZIMA**

- Rimu mbili plain A4 ONE
- Ndoo ndogo 2(moja ya shule, 1 kwa matumizi yake)
- Counter books 3Quire kumi na moja(11), kalamu na begi lake
- Dictionary (Oxford students' dictionary,) iwe ya kingereza –kingereza.
- Jembe lenye mpini.
- Fagio la chelewa au soft broom
- Sanduku la bati lenye kufuli (Tranka)
- Scientific calculator 01

**VIFAA VYA CHAKULA**: Mwanafunzi anatakiwa aje na sahani, kijiko na kikombe. Kwa ajili ya matumizi ya chakula hivyo atawajibika kuvitunza mwenyewe.

**WANAFUNZI WA BWENI**: Watatembelewa na ndugu zao wanaotambuliwa na shule, Jumamosi ya mwisho ya kila mwezi tu. Hakuna ruhusa ya kumtembelea siku isiyotajwa. Taarifa yoyote inayomhusu mwanafunzi kama vile vifo n.k. zifike kwanza ofisini kwa Mkuu wa shule au Makamu Mkuu wa Shule. Kila mzazi au mlezi atoe namba za simu shuleni kwa mawasiliano.

**RATIBA YA SHULE:**
Masomo yanaanza saa mbili 2.00 hadi saa kumi na nusu 10:30 jioni kwa siku za Jumatatu hadi Ijumaa. Siku za Jumamosi ni saa 2:00 hadi saa 7:50 mchana.

**WASTANI WA SHULE KITAALUMA KWA KILA SOMO NI ALAMA (50)**

**CHAKULA MAALUM**:
Shule haitoi chakula maalum (special diet) kwa wanafunzi wenye matatizo.

FOMU YA TAARIFA YA DAKTARI

Fomu hii ijazwe na Daktari anayetambulika baada ya kumfanyia mwanafunzi vipimo vilivyoelezwa na aje nayo mara anapojiunga na shule.

Fomu hii ya kujiunga itaambatana na sheria za shule pamoja na sehemu ya kujaza ya ahadi ya mwanafunzi na mzazi baada ya kusoma kila kitu kwa umakini.

**NB**: Unapofika shuleni tafadhali njoo na fomu hii tayari kwa usajili.

Karibuni sana

……………………..
C. SIARA
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA KILUTHERI EMBEKO
S.L.P 198 KONDOA

KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA (K.K.K.T)
DAYOSISI YA DODOMA
SHULE YA SEKONDARI EMBEKO
S.L.P 106, KONDOA
E-mail: embekolutheran@gmail.com
Mob. 0786-853890/0764-581739
Website.www.embeko.org

---

The medical officer

………………………………

………………………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR**……………………………………………………OF FORM ……………

Please examine the above mentioned student and complete

Thank you.

…………………
siara.c
HEADMASTER

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA KILUTHERI EMBEKO
S.L.P 106 KONDOA

# MEDICAL EXAMINATION FORM

## PART I: PERSONAL PARTICULARS (To be filled by the candidate)

Surname………………………… Other names……………………………………. Age ………………

Sex…………… Combination……………… School……………………………

**PART II: PERSONAL HISTORY**

(To be filled by medically qualified and registered professional)

Are you suffering of have you suffered from any of the following? Indicate **Yes** or **No**

Tuberculosis…………………………… Epilepsy…………………………

Asthma……………………………… Deformity………………………

Rheumatic fever……………………… Mental illness…………………

Allergic disorders…………………… Eye disorder……………………

Heart disease………………………… Ear, Nose, Throat disorder……………

Gastric or duodenal ulcers………… Skin disease……………………

Jaundice ……………………………… Anemia…………………………

Dysentery…………………………… Varicose veins…………………

Kidney disease……………………… Diabetes…………………………

Gynecological disorder……………… Any other serious disorder (specify)……………

**PART III: PHISICAL EXAMINATION**

Height (cm) …………………………………………………

Skin…………………………………………………………………

Weight (kg)…………………………………………………

Eyes: Conjunctive………………….. Pupil……………… Vision Right…………… Left…………………

Ears (state if any discharge)………… ………….. Mouth/throat………………………………

Nose……………………………… …………. Respiratory system…………………………

Abdomen………………………………………Any abnormality……………………………..

Cardiovascular system…………………..… Blood pressure ……..…………………………..

Systolic ……………………………….…Diastolic…….…………………….………………

Heart: Any murmur ……………………..........Arteries veins …………………………….……

**PART IV: LABORATORY**

Urine: Albumin…………………………………… Sugar…………………………………..…………

Leucocytes……………………………………….. Schistosoma……………….. ………………………..

Stool: Special emphasis on hookworms or Schistosoma……………………………..…………………

Blood examination

Hb level…………………………………………………………………………..

Neutrophil…………………………………………………………………………..

Eosinophils…………………………………………………………………….....

Basophiles………………………………………………………………..……..

Lymphocytes……………………………………………………………..……..

Monocytes………………………………………………………………..……..

ESR…………………………………………………………………...…….

Serology Widal test ………………………………… VDRL…………………..………….

Pregnancy test…………………………………………………………………………..

Additional information.

Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases………………………..…………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

I certify that I have examined the above named student and found her fit/not fit for school admission due to:-

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

Name……………………….…………… Signature…………………..……… Designation……………..

Date………………..………. Rubber stamp……………………………..

**Note: Student should bring the Completed form to school /Mwanafunzi ailete fomu hii shuleni ikwa imejazwa KIKAMILI**

## SHERIA ZA SHULE

1. Kuhudhuria parade ni LAZIMA. Kutokuhudhuria ni kosa la kinidhamu na kitaaluma. Usipohudhuria bila kibali cha walimu, utalazimika kuja na mzazi wako.
2. Mwanafuni ni lazima awahi shule. Kwa mwanafunzi wa kutwa, afike shuleni 6:45 asubuhi.
3. Kila mwanafunzi anapaswa kushiriki kwa ukamilifu kazi zinazotakiwa katika eneo alilopangiwa.
4. Ni marufuku mwanafunzi kuonekana nje ya darasa wakati wa masomo bila sababu maalum.
5. Utii kwa kengele ni jambo la lazima.
6. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vya dini na kuishi kwa kuzingatia maadili ya dini ya Kikristo.
7. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali.
8. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kuonekana nyumba za vileo, kumbi za starehe au nyumba za kulala wageni.
9. Wanafunzi wote wa bweni watavaa sare zao wawapo nje ya shule.
10. Wanafunzi hawaruhusiwi kupiga kelele wawapo maeneo ya kitaaluma shuleni.
11. Wanafunzi wa bweni watatembelewa na jamaa zao walioandikishwa kwenye fomu ya usajili kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi tu.
12. Ni marufuku kuvaa mavazi yasiyo ya shule. Mapambo si sehemu ya sare ya shule. Blauzi na mashati yatavaliwa kwa kuchomekewa.
13. Uvivu nje na ndani ya darasa ni kosa. Mwanafunzi atakayekosa kufanya mtihani kwa uzembe atakuwa amejiondoa shuleni mwenyewe.
14. Kukosa kuingia darasani kwa visingizio hakutavumilia.
15. Kutofika shuleni kwa wakati shule inapofunguliwa ni kosa linalostahili adhabu. Mzazi au mlezi ataitwa kumchukua mwanae.
16. Mwanafunzi asiyeonyesha bidii ya kujifunza si sehemu ya Jumuiya ya Shule ya Sekonari ya Embeko na atajifuta shuleni mwenyewe.
17. Ulevi wa aina yeyote ni kosa la kumuondoa mwanafunzi shuleni bila mjadala.
18. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwenzake mtumishi au mtu yeyote. Kosa hili halitajadiliwa.
19. Lugha chafu, ujeuri, kupigana, kudanganya na kuharibu mali za shule kwa makusudi kutamwondoa mwanafunzi shuleni.
20. Simu za mikononi ni marufuku mwanafunzi kumiliki, akibainika atanyang'anywa na kufukuzwa shule.
21. Kuingia au kuzurura maeneo ya jikoni ni kosa.
22. Wizi na udokozi ni makosa yasiyosamehewa.
23. Uchochezi wa mgomo na kufanya mgomo ni kosa la kukuondoa shuleni.
24. Mwanafunzi haruhusiwi kuoa au kuolewa.
25. Ni marufuku mwanafunzi wa kiume kuonekana maeneo ya bweni la wasichana. Aidha, msichana kuonekana maeneo ya bweni la wavulana.
26. Hakuna ruhusa kwa mwanafunzi yeyote kuwa msemaji wa shule labda kwa kuruhusiwa na uongozi wa shule.
27. Mwanafunzi akikosa shule bila taarifa atawajibika kuja na mzazi wake.
28. Mwanafunzi akikosa shule kwa mwezi mmoja atakuwa si mwanafunzi tena.

29. Ni marufuku kubandika picha za aina yeyote juu ya kuta za madarasa au vyumba vya kulala au kuchafua mazingira kwa jinsi yoyote ile.
30. Ni marufuku kwa mwanafunzi kudharau bendera ya taifa, wimbo wa taifa na wimbo wa shule.

**MAKOSA YAFUATAYO HUMFUKUZISHA MWANAFUNZI BILA ONYO**

1. WIZI WA AINA YEYOTE
2. UASHERATI, USHOGA NA UBAKAJI
3. ULEVI WA AINA YEYOTE
4. UVUTAJI SIGARA, BANGI NA MADAWA YA KULEVYA
5. KUPIGANA NA KUPIGA
6. KUHARIBU KWA MAKUSUDI MALI YA SHULE
7. KUOA NA KUOLEWA
8. KUPATA MIMBA NA KUTOA MIMBA AU KUMPA MSICHANA MIMBA
9. KUDHARAU BENDERA YA TAIFA, WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA SHULE
10. KUTOROKA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA KILUTHERI EMBEKO
S.L.P 196 KONDOA

# KIAPO CHA MWANAFUNZI NA MZAZI WAKE

(*Kiapo hiki ni mkataba kati ya mwanafunzi pamoja na mzazi wake na Shule ya Sekondari ya Embeko. Kwa kutia saini, inathibitisha kuwa watia saini wanakubaliana na taratibu zote za shule kama zilivyoainishwa kwenye Fomu ya Kujiunga na Shule ya Sekondari ya Embeko)*

## 1. AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi……………………………………..……. Mzazi/Mlezi wa …… Ninakiri kuwa nimezisoma sheria za shule nikiwa na mwanangu, tumezijadili kwa pamoja na tumezielewa.Ninakubali kushirikiana na uongozi wa shule katika kila kipengele cha malezi ya mwanangu,na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayoamuliwa na uongozi wa shule pale mwanangu atakapokiuka mojawapo ya sheria na kanuni hizi.Nitalipa ada,michango ya shule, na kuheshimu maelekezo mengine yanaytolewa na shule.

Saini ya mzazi/mlezi……………………………… Tarehe:………………..

## 2. AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi ………………………niliyechaguliwa kujiunga na kidato cha …….. katika sekondari ya Embeko,nimesoma kwa makini sheria na taratibu za shule nikiwa na wazazi/walezi wangu. Nimejadiliana nao na nimezielewa vema kabisa. Ninahidi kuzitii, kuziheshimu na kuziishi wakati wote bila kusukumwa na nitakuwa tayari kuchukuliwa hatua kali za kinidhamu na uongozi wa shule endapo nitakiuka mojawapo ya sheria na kanuni hizi.

Saini ya mwanafunzi:……………………… Tarehe:………………………..

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA KILUTHERI EMBEKO
S.L.P 198 KONDOA